TANGAZO LA SERIKALI NA. 552 la tarehe 26 Jul 2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 28(1)(d))*

AMRI YA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MAKETE ("MAKETE WSSA"), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii litajulikana kama, Amri ya Marekebisho ya Bei ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete ("MAKETE WSSA") ya mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Agosti 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Makete WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 31 Oktoba 2019 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete itawaunganisha wateja wake wote na dira za maji ifikapo 2020/21;

(c) Mamaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete ihakikishe kuwa

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(d) ifikapo tarehe 31 Oktoba au Kabla, Makete WSSA iandae mpango wa kutambua makundi yenye mahitaji maalum na kuweka mfumo wa kuwapatia makundi hayo huduma ya maji kwa unafuu zaidi. Makete WSSA inapaswa kuijulisha EWURA kuhusu uandaaji na utekelezaji wa mpango huo;

(e) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(f) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(g) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne; na

(h) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete itaendelea

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete katika siku zijazo.

Kufutwa kwa Amri Na. 11-014 la mwaka 2011

5. Amri hii inafuta Amri Na. 11-014 katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Makete.

**JEDWALI**

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

## JEDWALI LA KWANZA

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 3)*

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali la 1(a): Bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa kwa wateja wenye dira (Shilingi/ mita ya ujazo)

| Aina ya mteja | Kiwango | Bei za sasa | Bei iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 0-5 | 345 | 800 | 900 | 1,000 |
| | >5 | 345 | 900 | 950 | 1,000 |
| Biashara | | 395 | 1,000 | 1,100 | 1,100 |
| Taasisi | | 345 | 1,000 | 1,090 | 1,100 |
| Viwanda | | 500 | 1400 | 2,100 | 2,100 |
| Magati | | 300 | 700 | 800 | 1,000 |

Jedwali la 1(b): Bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa kwa wateja wasio na dira (Shilingi/ Mwezi)

| Aina ya mteja | Bei za sasa | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 4,500 | 7,000 | Haijaidhinishwa | |
| Taasisi | 15,000 | 36,000 | | |
| Biashara | 7,500 | 14,000 | | |
| Viwanda | 17,000 | 44,000 | | |
| Magati | 22,000 | 28,000 | | |

Jedwali la 1(c): Ada ya sasa na iliyoidhinishwa ya maunganisho ya maji safi (Shilingi/maunganisho)

| Kundi la wateja | Ada ya sasa | Ada zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| Majumbani | 20,000 | Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi kama ilivyobainishwa katika kanuni za Majisafi za mwaka 2013 |
| Taasisi | 30,000 | |
| Biashara | 30,000 | |
| Viwanda | 35,000 | |
| Magati | 22,500 | |

Jedwali la 1(d): Ada ya sasa na iliyoidhinishwa ya kurejeshewa huduma ya maji baada ya kukatiwa (Shilingi/kurejeshewa huduma**)**

| Aina ya mteja | Bei za sasa | Ada zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 5,500 | 12,000 | 12,000 | 12,000 |
| Taasisi | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 5,500 | 20,000 | 15,000 | 15,000 |
| Magati | 5,500 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

## JEDWALI LA PILI

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(e))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Kazi zitakazotekelezwa | Shilingi za Kitanzania (Milioni) | | | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Matengenezo | | | | |
| Ukarabati wa bomba kuu kutoka Ludihani hadi tenki la Ngiu Ndulamo, Ujenzi wa chemba 3 za valvu ya kusafisha bomba (washout), ujenzi chemba 3 za valvu ya kutolea hewa, ukarabati wa bomba umbali wa km 1.2 pamoja na kujenga alama mahali ambapo bomba limepita. | 5.0 | 6.0 | 5.0 | Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022 |

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

| Kazi zitakazotekelezwa | Shilingi za Kitanzania (Milioni) | | | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Ukarabati wa bomba kuu kutoka Kidwiva hadi tenki la Mwongolo, ujenzi wa chemba 4 za kusafisha bomba (washout), ujenzi wa chemba 3 za valvu ya kutolea hewa, ujenzi waalama za kuonyesha bomba (marker post) | 6.0 | 7.0 | 5.0 | Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022 |
| Ukarabati wa bomba kuu kutoka chanzo cha Ivalalila hadi tanki la Mwongolo, ujenzi wa chemba 1 ya kusafisha bomba (washout), ujenzi wa chemba 1 ya valvu ya kutolea hewa, ujenzi waalama za kuonyesha bomba (marker post), kuhamisha bomba umbali wamita 800. | 6.0 | 5.0 | 8.0 | Utekelezajiutafanyikakablayatarehe 30 Juni, 2022 |
| Ukarabati wa matenki ya maji: Tenki la Mwongolo A, kupiga plasta, kujenga uzio, kujenga paa la tenki pamoja na ujezi wa sehemu ya kuweka dawa kwenye maji.<br>Tenki la Mwongolo B, kupiga plasta pamoja na ujezi wa kibanda cha mlinzi.<br>Tenki la Ngiu: ujenzi wa sehemu ya kuweka dawa kwenye maji, ujenzi wa geti pamoja na ngazi ya tenki. | 18.0 | 20.0 | 24.0 | Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022 |
| Ukarabati wa matenki 4 ya kupunguza msukumo wa maji (BPT) pamoja tenki 1 dogo la kuhifadhi maji (Mpangala na Mwongolo BPT-kupigaplasta, Ludihani BPT –kukarabati uzio, matenki madogo (BPT) Kitunuli na Ndulamo- ujenzi mpya) | 10.0 | 14.0 | 16.0 | Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022 |
| Jumla Ndogo (Matengenezo) | 40.0 | 46.0 | 53.0 | |
| UwekezajiMpya | | | | |
| Kuongeza mtandao wa mabomba kwa umbali wa km 9.2; Kutoka Kona hadi Chamani km 1.25, Kutoka Hospitali hadi Manzese km 1.6, Sabasaba hadi Mahakama km 1.5, Ndulamo km 1.6, Mpangala 0.65 na Kitunuli km 1.5 | 20.0 | 24.0 | 22.44 | Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022 |

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

| Kazi zitakazotekelezwa | Shilingi za Kitanzania (Milioni) | | | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Ujenzi wa ofisi mpya (Kuweka paa pamoja na vifaa vya kumalizia ujenzi, ununuzi wa samani, kuweka uzio na kupata hati ya kiwanja) | 50.0 | 50.0 | | To be implemented by 30th June 2020 |
| Ununuzi wa tarakinishi ‘Computer” 4 za ofisi pamoj ana vifaa vyake, ununuzi wa samani za ofisi, ununuzi wa pikipiki 2, na vifaa vya kufanyia kazi | 10.0 | | 20.0 | |
| JumlaNdogo – Uwekezaji Mpya | 80 | 74.0 | 59.0 | |
| JumlayaUwekezaji Wote | 120.0 | 120.0 | 112.0 | |

**JEDWALI LA TATU**

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(f))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Kiwango cha asilimia ya idadi ya watu wanaohudumiwa na Mamlaka ya Maji safina Usafi wa Mazingira Makete | % | 66 | 74 | 80 |
| Kiwango cha idadi ya watu wanaoishi katika eneo lililofikiwa na mtandao wa maji | % | 68 | 67 | 71 |
| Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) | % | 32 | 30 | 28 |
| Wastani wa muda wa utoaji huduma | saa | 20 | 22 | 24 |
| Kiwango cha Wateja wa Dira | % | 95 | 100 | 100 |
| Kiwango cha Ufanisi wa Ukusanyaji mapato | % | 90 | 95 | 98 |

*Tangazo la serikali na 552. (linaendelea.)*

**JEDWALI LA NNE**

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 4(g))*

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (TZS)

| Maelezo | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|
| UndeshajinaMatengenezo | 138,420,000 | 194,260,000 | 213,920,000 | 240,610,000 |
| Uchakavu | 55,000,000 | 94,520,000 | 92,980,000 | 84,310,000 |
| FaidayaUwekezaji | 3,180,000 | 25,480,000 | 27,020,000 | 27,690,000 |
| JumlayaMahitajiyaFedha | 196,600,000 | 312,250,000 | 333,930,000 | 352,610,000 |
| Ondoa: MapatoMengineyo | 1,700,000 | 12,000,000 | 12,000,000 | 12,000,000 |
| MahitajiyaFedhakutoka Mauzoya Maji | 194,900,000 | 300,250,000 | 321,930,000 | 340,610,000 |
| Uzalishajiwa Maji (mita za ujazo) | 310,000 | 430,000 | 450,000 | 450,000 |
| Upotevuwamaji (%) | 38 | 32 | 30 | 28 |
| Maji yaliyouzwa ($m^3$) | 192,200 | 292,400 | 315,000 | 324,000 |
| Wastaniwa Bei (ShilingikwamitayaUjazo | 1,014 | 1,020 | 1,020 | 1,050 |

Dodoma
............................ 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*